# DHIMA YA METHALI KATIKA MALEZI

S.A.K. Mlacha

## 1. UTANGULIZI

Methali zimejaa maadili ambayo humsaidia mwanadamu kwa kumwongoza kwenye misingi bora ya maisha. Zinaweza kuwa ni za masuto au mauidha. Methali za mauidha ni zile zenye lengo la kuonya, kuusia, kushauri au kufunza. Methali za masuto nazo zina lengo hilo hilo, lakini maneno yake ni ya kukaripia, na hata kukemea. Ni makali masikioni na katika lugha ya kawaida huonyesha dalili ya utovu wa heshima au lugha ya adabu. Pia huwa hayatumiki katika halaiki au mbele ya watu wazima au wageni.

a) Methali ya mauidha: "Nasikitika, Bi Jarifa, tumeshindwa kuua ndege wawili kwa jiwe moja." Anaanza kunieleza kwa fumbo. ----- (*Nitamshitaki kuzimu*, uk. 44).

b) Methali ya Masuto: "Usiige kunya kwa tembo utapasuka msamba."

au

"Kupenda kidonda na usaha wake" (*Nitamshitaki kuzimu*, uk. 18)

Hivyo methali za mauidha na masuto, zote zimelengwa kwenye ukweli wa maisha. Zimetolewa ili kutoa maonyo, fundisho na kusaidia kurekebisha tabia za watu wa jamii moja. Hali hizo katika riwaya za Kiswahili zimejitokeza kwa namna tofauti. Namna hizo za kutolea methali zinasaidia kuonyesha uhalisi wa matumizi ya methali. Pia zitakuwa ni njia mojawapo za kuweza kuona umuhimu wa methali katika

maisha, kuangalia nyanja zinazofumbatwa na methali katika malezi. Malezi yanaweza kufanikiwa kwa kutumia maneno mazuri au makali. Ndiyo maana methali zimeangaliwa kwa upande wa mauidha na masuto. Mauidha yanaweza kujumuisha hali ya kupongeza na kuunga mkono jambo, kufariji na kutia jitihada. Masuto yanaweza kuwa na nia ya kushambulia matendo mabaya, kutaka kumrekebisha mtu na hata kukejeli. Hivyo dhima ya methali katika riwaya itajitokeza kama dhima ya methali kwenye kumrekebisha mwanadamu na kumjenga mwanadamu chini ya misingi muhimu ya matakwa ya jamii yake. Hapa tutaonyesha jinsi riwaya zinavyotumia methali ili kutoa picha ya maisha halisi.

## 2. DHIMA ZA METHALI

### 2.1 Kufunza/Kulea

Dhima kuu ya methali ni kumfunza, kumlea na kumfanya mtu awe mtu, kumfanya mtu aoane na matakwa ya jamii yake. Jukumu la malezi ni kubwa sana, kwa watoto hata wazee, hivyo matumizi ya methali huukumba umri wote wa binadamu. Papo hapo, methali hutumia mbinu tofauti kufikia lengo hilo, licha ya kwamba muundo wake na namna zinavyotumiwa ni njia nyingine za kukidhi dhima ya methali kisanii.

### 2.2 Kashifa

Katika kashifa, mtu husimulia habari za kumvunjia mtu heshima yake au kutoa siri ya kuaibisha. Katika maisha ya mwanadamu hali hii huweza kujitokeza kwenye mahusiano yao. Kashifa katika methali aghalabu huwa sio rahisi kuigundua. Zipo methali zinazotoa kashifa wazi kama vile, "masikini akipata matako hulia mbwata." Nyingine ni zile ambazo kashifa inajitokeza baada ya kuchunguza methali yenyewe kwa ndani zaidi. Kwa mfano:

> "...mangapi umewatenda
>
> Umemsahau Farashuu na mwanawe?
>
> Mwiba uchomeako ndiko utokeako.
>
> Na huu Bwana Masudi ni mwanzo -
> ...ni mwanzo tu." Kazija alikupuka.
> (Utengano. uk. 15).

Bi Kazija alikuwa anamkashifu Maksudi kwa matendo yake mabaya. Anamkumbusha matendo yake kwa kutumia methali, papo hapo akidhihirisha na kuhalalisha kitendo alichomfanyia mzee huyo. Ukweli na hekima iliyopo ndani ya methali hiyo ni fundisho kubwa kwa Maksudi. Bi Kazija ameitumia methali kuonyesha ubaya wa mabaya.

## 2.3 Kejeli

Kumkejeli mtu ni kumsema kwa maneno ya dharau, kwa kufanya mzaha na kumsimanga. Kejeli inayokuwepo kwenye methali huonyesha zaidi kutofaulu kwa matendo. Baada ya mtu kufanya kitendo akidhani atafanikiwa, anashushuliwa na yule anayeshuhudia kutofanikiwa kitendo hicho. Kwa mfano methali ya mwenda tezi na omo hurejea ngamani katika Utengano ni kejeli.

> "Chatu mtu likasita, likatoa ulimi na kuchekacheka. Mbio za sakafuni huishia ukingoni, sauti lake kama radi! Mbio zako zimefika wapi?" (uk. 133)

Hapa joka hilo lilikuwa linamkejeli Maimuna na kumsuta kuwa jitihadi ya kukimbia haikumfikisha popote. Mfano mwingine wa kejeli: "kubwa ni analolijua mtu mwenyewe, mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi" (Utengano uk. 154). Maimuna ni mwingi wa methali. Hivyo kwa kutumia kejeli hii, mhusika hupata funzo kwa yale aliyoyatenda na kuweza kujirekebisha.

## 2.4 Kushutumu Matendo

Mojawapo ya kazi muhimu ya matumizi ya methali katika riwaya ni kushutumu matendo. Matendo yote mabaya yanashambuliwa na methali nyingi tu. Katika riwaya, kipengele hiki cha matumizi ya riwaya kinaongoza. Mojawapo ya sababu ya kuongoza huko ni kwa vile riwaya nyingi zinayaona na kuyaelezea matendo mabaya katika maisha ya binadamu. Riwaya zinakabiliwa na matendo hayo na kuyapatia sahihisho, ambalo ni methali hizo. Kwa mfano, katika riwaya ya Thamani ya Ukubwa, Rinda Musekusi amepewa wadhifa mkubwa sana. Anatumia wadhifa huo aliopewa ili kuliangusha taifa na kuhujumu uchumi wa nchi. Baadaye anafikishwa mahakamani na kuhukumiwa kifungo cha maisha. Kabla ya hukumu hiyo, hakimu anamwambia yafuatayo:

> "kama mtoto asiye shukurani, apigaye mateke tumbo la mamake kwa kukosa adabu"; wewe umelifanyia taifa lako hivyo hivyo. Kama punda ashibaye -----. Ndivyo, ni kweli kama wahenga walivyosema, fadhili ya punda ni mateke" (uk. 81-82).

Hapa methali hiyo inashutumu kitendo cha Rinda. Matendo yake yote mabaya yamefumbatwa ndani ya methali hiyo.

## 2.5. Kuonya/Kutahadharisha

Katika jamii watu huona na kuyapima matendo ya wengine wakati mwingine hata yao. Wanaweza kuyaangalia na kuona matokeo yake muda ujao. Ionekanapo kuwa matendo hayo yanaweza kuleta ubaya au maudhi (kwa jamii au mtendaji), methali zinakuwepo tayari kutoa maonyo na kumtahadharisha mtendaji. Mtendaji anapewa picha ambayo anaweza kuilinganisha na matendo yake na kisha kujua madhara ya matendo hayo, mifano iliyowekwa kwenye methali inakuwa imejikita kwenye hekima na falsafa ya maisha. Kwa mfano methali ya Asiye sikia la mkuu, huvunjika guu. Au mfano mwingine kutoka kwenye riwaya ya Umelogwa au Umetumwa? iliyotolewa hivi:

> "Kwa kweli mtu huyu nilikuwa namfahamu sana; licha ya kumfahamu, alikuwa rafiki yangu mkubwa sana; lakini kikulacho ki nguoni mwako. Kumbe rafiki yangu -----" (uk. 35).

Methali za kuonya na kutahadharisha zinaweza kutumiwa kwenye kujikosoa na kujuta pia. Methali hizi humfanya mtu aweze kuyaona yale yanayoweza kumfika na hivyo kuweza kujitahadharisha mapema.

## 2.6 Kufariji/Kuliwaza na Kupongeza

Katika maisha wanadamu hukumbukana na matatizo kemkem. Mengi ya matatizo hayo yanaweza kukatisha tamaa malengo fulani au kuzidisha mawazo. Hali hizo zote zinarudisha nyuma maendeleo ya mwanadamu. Kwa msaada wa ufahamu wa kuwa hali hizo sio ngeni kwenye maisha, methali zimejitokeza ili kujaribu kutuliza matatizo hayo. Zimeweza kuchukua nafasi ya kumfariji mwanadamu na kumpa nafasi ya kujaribu tena, kujiona hayuko peke yake na

kutulizwa roho. Kwa mfano tuangalie katika riwaya ya Nyota ya Rehema (uk. 19). Aziza anajikuta kwenye lindi la matatizo, hasa baada ya mumewe kuoa mke mwingine. Mama yake anayaona matatizo aliyo nayo Aziza na anaamua kumfariji binti yake. Hivyo anaelezea mambo yaliyomtokea na kuyabanza na methali kama ifuatavyo:

> ".... Siku za awali lilianguka shindo la ndovu kumla mwanawe, mimi nikatupiliwa mbali. Lakini nikaubana. Najua, mwenda tezi na omo Ngamani. Unadhani ilikuwa nini? Aliwatupia mmoja mmoja akarejea kwangu. Na leo yu wapi?"

Methali ya mwenda tezi na omo marejeo ngamani imetumiwa kama mbinu ya kuweza kukita faraja na maliwazo. Kuweza kumtuliza Aziza na kumuonyesha wazi kwamba mambo hayo huwa yanatokea kwa wengine pia, hivyo asiwe na mawazo mengi. Hivyo aliishi na kusubiri, hadi alipokufa. Hata hivyo lengo lilikuwa kumfanya Aziza aweze kuwa na subira, awe mvumilivu katika maisha.

Zaidi ya kufariji na kuliwaza, methali zinaangalia upande mwingine pia. Huwa zinaona matendo mazuri na umuhimu wa kupongeza na kuongeza moyo wa kutenda hivyo kwa yule aliye tenda. Methali kama kidole chema huvishwa pete ni kati ya methali zinazoonyesha sifa, pongezi na hongera kwa mtenda mazuri.

## 2.7 Kuhimiza

Kwa vile methali zinaongelea matendo ya wanadamu, hali ya kuhimiza na kutia juhudi katika matendo ni muhimu. Methali zina nafasi kwenye kuhimiza wanadamu wasikate tamaa ili kufikia malengo yao. Zinaweza kumpa mtu nia zaidi ya kufanya jambo na moyo wa kutegemea mafanikio, kuongeza jitihada, na kukubali kukabiliana na hali nzito. Uwezo huu wa methali unakuwa na manufaa zaidi hasa kwenye shughuli za ujenzi wa taifa, kitaaluma, kiuchumi na hata katika kukabiliana na vipingamizi vya kisiasa.

Kwa mfano, methali ya Mtaka cha mvungu sharti ainame. Methali hii huwa na uzito zaidi kuliko kumwambia

mtu kwa mfano kuwa "kama unahitaji kitu, jishughulishe." Katika methali upo uzito wa hekima na mantiki licha ya ukweli wa methali hiyo. Methali ya Bandu bandu humaliza gogo nayo pia hutoa picha yenye ukweli, ambayo inaweza kumfanya mtu aweze kuongeza jitihada, akiamini kwamba upo mwisho, na mwisho huo utakuwa ndio mafanikio yake. Hivyo methali zinaweza kumhimiza mtu na kumfanya aongeze jitihada na kutegemea mafanikio katika matendo na malengo yake. Ni njia mojawapo ya kuweza kuleta maendeleo kwa kuhimiza ufanyaji kazi. Kuleta maendeleo kwa kuhimiza ufanyaji kazi ni shughuli mojawapo ya malezi ya binadamu na jamii.

## 2.8 Tabia/Uhusiano

Wakati mwingine wajumbe wa jamii wanaweza kushuhudia mwingine anavyopotoka. Methali inaweza kutumiwa katika jitihada ya kumnyoosha au kumfanya aingie na kufuata mfumo wa jamii yake. Methali hiyo inaweza kumfahamisha mtu huyo kwamba upo ubaya utakaojitokeza. Mojawapo ya methali za aina hiyo ni Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu. Asiyefunzwa na mamake, hufunzwa na ulimwengu. Tabia ya kutosikiliza au kutolelewa vizuri inapatiwa njia nyingine ya kujirekebisha, ambayo nayo ni njia ya malezi pia.

Methali zingine hutoa picha ya uhusiano baina ya watu. Zinaweza kuonyesha hisia fulani za undugu au urafiki. Kwa mfano methali ya Damu nzito kuliko maji kwenye Sudi ya Yohana. Methali za aina hii zina dhima ya malezi ya udugu na urafiki. Humlea mtu kwenye utu na ujamaa.

# 3. MUUNDO WA METHALI

Sentensi ya methali ina muundo wake pekee. Muundo huo husaidia kutofautisha methali na sentensi zingine. Tunaweza kuugawanya kwenye sehemu mbili muhimu. Mpangilio na maudhui. Sehemu hizi mbili zinachangia kuzatiti dhima kuu ya methali, husaidia kuzifanya methali zikumbukwe kirahisi na kueleweka fundisho lake. Methali imepangwa katika sehemu mbili na kila sehemu ina maudhui yake na inatoa picha yake maalum. Picha ya sehemu moja sio huru bila kuunganishwa na picha ya sehemu ya pili.

## 3.1 Mpangilio

Mpangilio wa sentensi za methali ni tofauti na mpangilio wa sentensi zingine. a) methali ni fupi sana. Ufupi wa sentensi hiyo umefumbata matendo mapana sana, yanayoweza kuelezeka kirefu kwa maneno ya kawaida. Hivyo iwapo matendo hayo yangeelezwa kwa urefu, yaani iwapo methali zisingekuwepo basi ingebidi kutumia sentensi nyingi zaidi ya moja. Kwa mfano:

> "Kaka Joseph, husemwa kuwa, ng'ombe avunjikapo guu malishoni, hurejea zizini: na kadhalika, damu nzito kuliko maji -----" (Sudi ya Yohana uk. 37)

Badala ya kutamka methali hizo na kueleweka, ingebidi Yohana aanze kuelezea kirefu; kwa mfano hivi: kaka Joseph, unajua mtu anapopatwa na shida hurudi nyumbani kwao ili aweze kupata msaada: na kadhalika utambue kuwa wewe ni ndugu yangu. Hata siku moja mimi sitafurahi kuona damu yako hiyo inamwagika, licha ya kwamba hatupatani. Damu yako hiyo siyo sawa na maji ambayo yanaweza kumwagika tu nisijali. Hata hivyo, maji ni mepesi, tena mepesi zaidi kuliko -----". Licha ya kwamba Yohana angeelezea kirefu hali ya methali hiyo, mtu mwingine naye angeifafanua kivyake kufuatana na hali ya suala lake.

Ufupi wa methali ni mpango ambao pia husaidia kuweza kuzikumbuka kwa urahisi zaidi na kuupata ujumbe wa maadili yake vyema. Hivyo, ambapo mtu angepaswa kukumbuka hadithi yote na kila lililotokea ambalo linaelekea kuwa sawa na hilo, methali imerahisisha. Yote haya (matendo) yamewekwa pamoja ili yaweze kuwakilisha funzo litokanalo na vitendo hivyo. Hivyo ni kama mkusanyo wa matendo mengi katika maneno machache. Khatibu M.S. katika makala yake:"Fani Katika Methali za Kiswahili" (Warsha ya Methali, iliyofanyika katika Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, 1981) amesisitiza kuwa "Ufupi wake na unyofu wa mstari mmoja haukutindikwa kimaana. Maana na falsafa iliyofumbatwa katika kila tindi la methali ina upana na uzito wa mawazo iwezayo kufasirika katika lukuki wa majarida na vitabu."

(b) Sentensi za methali kwa kawaida huwa hazibadiliki. Maneno yanayoifanya sentensi ya methali kuwa kamili, mara nyingi ni yale yale. Yanapobadilishwa au

mpangilio wa maneno hayo unapobadilishwa ni pale msanii anapokuwa na lengo maalum au nia nyingine tofauti kama sio kutoijua methali. Kwa mfano methali ya Baada ya dhiki faraja imetolewa kwa nia maalum katika Nyota ya Rehema;

> "-----Maisha yalimfunza kuwa kila baada ya dhiki faraja na kila baada ya faraja dhiki vile vile." (uk. 161).

Hapa msanii kafanya hivi makusudi ili kuonyesha pande zote mbili za maisha, kisanii. Hata hivyo ipo mifano, japo michache, ya methali zenye utata. Utata huo hutokana na kubadilishwa kwa sehemu fulani za maneno ya sentensi ya methali. Mpangilio unabakia pale pale. Maneno ni yale yale isipokuwa sehemu kadhaa zinabadilika. Kwa mfano:

1. "Ng'ombe avunjikapo guu malishoni, hurejea zizini" (Sudi ya Yohana. uk. 37).
2. "Ng'ombe akivunjika mguu malishoni, hujikokota zizini kusaidiwa" (Kusadikia. uk. viii).
3. Ng'ombe avunjikapo guu, hurejea zizini" (Gamba la Nyoka. uk. 137).

Riwaya zote hizi tatu zinaonyesha tofauti ya muundo wa maneno ya methali. Hata hivyo, maneno ni yale yale na maana haikubadilika. Tofauti hii ni ya kisanii tu.

c) Methali zina sehemu mbili muhimu. Kila sehemu huzingatia jambo fulani, ambalo linaifanya methali iweze kukamilika. Sehemu ya kwanza inaweza kutumika badala ya methali nzima kutamkwa. Lakini sehemu ya pili sio kila mara inasimamia methali nzima. Zipo methali ambazo utajapo sehemu ya pili tu, hazieleweki. Kwa mfano tuchukue methali ya Mtaka cha mvunguni sharti ainame. Mtu asemapo mtaka cha mvunguni ----- methali nzima itakuwa imeeleweka. Pia hata asemapo ----- sharti uiname kiasi mtu anaweza kuelewa methali hiyo nzima. Lakini methali kama Mwenda pole, hajikwai, Mtoto wa nyoka ni nyoka kwa mfano, hazitaeleweka iwapo tutachukua sehemu ya pili tu. Kwa mfano '----- ni nyoka' au '----- hajikwai'. Hii inasababishwa na hali zifuatazo:

Kwanza, sehemu ya kwanza kila wakati inakuwa ndefu zaidi ya sehemu ya pili. Urefu huo unasababishwa na kuwa kwake chanzo cha methali. Kama chanzo cha methali sehemu

hiyo inapaswa kufafanua zaidi hali ambayo imetendeka na inastahili kuangaliwa ili irekebishwe. Ndicho kiini cha methali na hapo ndipo yalipo matendo ambayo hayastahili kutendwa au yanayostahili sifa. Sehemu ya pili ni fupi kuliko ya kwanza. Hapa ndipo kwenye matokeo ya kufanya vile ilivyoelezwa kwenye sehemu ya kwanza. Ni jibu la matendo au maono ya sehemu hiyo ya kwanza. Kuna methali chache zinazokiuka mpangilio huu. Mfano wa hizo ni "Hasira hasara." Methali hii imegawanyika sawa. Sehemu ya kwanza inaongelea hasira ya pili ubaya wa kuwa na hasira kwamba ni hasara. Mifano mingine ni mtupa jongoo, hutupa na mti wake au uzuri wa mkakasi, ndani kipande cha mti. Methali hizi zinaonyesha kuwa sehemu ya kwanza ni fupi kuliko sehemu ya pili. Hata hivyo, maudhui yake yanabaki pale pale, kuwa sehemu ya pili ni tegemeo la kwisha kufanya hivyo, matokeo ya kitendo cha aina hiyo.

Hivyo basi, tunaweza kusema jamii ya kiswahili, kwenye methali huangalia pande mbili za maisha ili kufanya hitimisho na kufanikiwa kumpa mtu maonyo, mwangaza wa maisha na fundisho.

## 3.2 Muundo Kimaudhui

Katika methali kuna sehemu mbili kimaudhui. Sehemu ya kwanza hutoa au huonyesha taswira ya mawazo ya jambo lililokwisha tokea. Sehemu ya pili inazingatia tegemeo la matokeo ya kutenda. Jumuisho au unganisho hili huleta picha kamili ya methali. Kwa mfano katika riwaya ya Maputo imetumika methali kama ifuatavyo:

> "Hata hivyo, ninakaza moyo na kuamua
> kuendelea na Operesheni Vinyazo vya
> Qhissanga Ovo, Operesheni ambayo
> nimekwisha kuianza kuishughulikia.
> Maji ukiyavulia nguo, ni lazima kuyaoga.

Picha tuipatayo katika methali hii ni ile ya maji na mtu pembeni, ambaye tayari ameshavua nguo ili aoge. Yaani picha ya mnuia kutenda kitendo fulani cha maana. Matayarisho ya kuanza kitendo hicho tayari na kilichobakia ni kutimiza. Sehemu ya pili ya methali ni tegemeo. Tegemeo tulipatalo kwenye methali hii ni kwamba, baada ya hali hiyo ya matayarisho, tunategemea mtu huyo aoge. Atende jambo lenyewe.

Muundo mwingine wa kimaudhui katika methali ni ule wa kutumia tamathali. Tamathali hutawala sana uumbaji wa

methali hasa kwa vile karibu zote zinatumia tamathali. Tamathali katika methali ni mada ambayo itachunguzwa baadae, pekee.

Muundo wa kimaudhui unaangalia vitendo viwili tofauti. Kitendo cha kwanza kinakuwa kimetayarishwa kama msingi. Kitendo cha pili kinategemewa kitokee iwapo cha kwanza kitafanywa. Hivyo Asiyesikia la mkuu huvunjika guu huonyesha kitendo cha kutosikiliza, ukaidi. Iwapo mtu hatasikiliza kuonywa, inategemewa kuwa yatamtokea mabaya. Hivyo ni muundo wenye fundisho ambalo limetokana na kitendo na adhabu ya kitendo hicho.

## 3.3 Methali na Ukweli

Methali zinaweza kuchukuliwa kama picha ya maisha kwa ufupi, ukweli wa namna ya kuishi na watu wa jamii yako. Lakini hata hivyo, ifahamike kuwa ukweli ni jambo lenye uhakika, kinyume cha uwongo. Methali hazisemi uwongo kimaudhui. Lakini kama sentensi zitamkwapo zinaweza kuonyesha hali ambazo sio za kweli katika maisha halisi, sentensi za methali zinaweza kuwa na ukweli hata kwenye maisha. Kwa mfano methali ya Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe au Ukitaka cha mvunguni sharti uiname. Maana sisisi ya methali hiyo inaonyesha ukweli. Mtu akipiga ngumi ukuta ni kweli ataumiza mkono wake. Lakini pia maana ya methali hiyo ni pana zaidi kuliko maana hiyo sisisi. Kutokana na ukweli wa maana sisisi inapatikana picha ya methali, fumbo lililojaa mwongozo wa maisha na ukweli wa matendo. Picha ambayo inampa mwanga mtu na kumelea kufuatana na ukweli uliowekwa kwenye sentensi hiyo.

Lakini zipo methali ambazo zitamkwapo hazionyeshi ukweli wowote. Methali hizi huonyesha ukweli wake kwenye matokeo tu ya kutendwa kitendo hicho. Methali kama vile Samaki mmoja akioza wote wameoza ni methali ambayo isikiwapo kama sentensi tu inaonyesha kwamba sio kweli. Kwenye hali halisi samaki mmoja akioza wengine bado ni wazima wanaendelea kuuzwa au kuliwa. Hivyo hapa methali haisemi ukweli, bali ichukuliwapo kama tamathali. Jumuisho hili limefanyika ili kumfanya mtu ajione katikati ya kundi, ahusishe matendo yake na jamii. Ajilee kwa misingi ya kijamaa.

Methali zingine zinaelezea mambo ambayo sio ya kweli bali yamelazimishwa kuwa hivyo. Kwa mfano, Fadhili ya punda ni mateke: Methali hii ni njia tu ya kukosolea.

Lakini ukweli ni kuwa punda hutupa mateke kwa sababu zingine, hasa kwa kubebeshwa mizigo au viboko na wala sio kutendewa wema. Kulishwa na kufugwa yote ni kwa lengo la kutumikisha na sio wema. Hali hii imelazimishwa ili kuleta picha ya shukrani.

Hata hivyo sio kila methali itumiwapo inatokea kuwa hivyo. Methali inaweza kutumiwa kwa lengo fulani lakini isitokee hivyo. Kwa mfano katika Nyota ya Rehema, Amina anafarijiwa na mama yake kuwa asijali tabia za mumewe kwani Mwenda tezi na omo-----. Lakini Amina hadi alipo-kufa mumewe wala hakubadili mwenendo. Hivyo wakati mwingine methali zinadanganya kwenye ukweli japo kimaudhui zina lengo zuri na linalotegemewa kuwa kweli. Hali hii inapingana na ile ya wanazuoni wanaoamini kwamba methali siku zote zinaweza kuchukuliwa kama vigezo vya kutolea picha ya matokeo ya kweli.

## 4. HITIMISHO

Kwa kuzingatia uchunguzi uliofanywa kwenye riwaya kadhaa za kiswahili, imedhihirika kuwa methali zina jukumu kubwa katika malezi ya jamii, katika lengo la kuunda jamii bora. Kila jamii inatambua na imeshuhudia makosa tofauti yanayotendwa na wanajamii. Njia ya kukabili hali hiyo inaweza kuwa kwa kutumia sheria za jamii, dini, au madaraka ya kijamii. Zaidi ya njia hizo, methali zimejitokeza kuwa ndiyo njia pekee ambayo inaweza kukabili hali tofauti za matendo ya jamii. Hasa tuangaliapo na kufahamu kuwa dini na sheria zina mipaka yake, wakati methali kama zilivyojitokeza katika makala haya, huzingatia uwanja mpana zaidi wa matendo hayo ya binadamu. Iwapo dini zina makundi maalum ya wahusika na waumini, methali zinawahusu watu wote, wa dini tofauti. Iwapo sheria zinapovunjwa adhabu yake imepimwa na wahusika, methali haipimi kiwango cha adhabu kwa yeyote anayevunja sheria hizo za jamii. Hakimu wa matendo kwenye methali ni matokeo ya matendo hayo. Hivyo basi, methali zinaweza kutumika zaidi katika malezi. Ni silaha bora zaidi ya malezi kuliko dini na sheria, hasa kwa vile zinamkumba mtu katika hali yoyote kama vile ya matendo mabaya, kinyume cha matakwa ya jamii. Methali ni njia mojawapo ya kujikosoa kwenye misingi ya kijamaa. Tofauti tu ni kwamba, uoga umpatao mhalifu kwenye methali haulingani na ule wa kufungwa (Sheria) au kuchomwa moto (Dini). Hata hivyo, mjamaa halisi si anayejifanya hivyo kwa wote, bali ni yule anayetambua misingi bora ya utu na maendeleo ya jamii yake.

MAREJEO


1. Chachage, C.S.L. (1981): *Sudi ya Yohana* DUP, Dar es Salaam

2. Keto, A.S. (1976): *Nitamshitaki Kuzimu* Pan-African Publishing Co., Dar es Salaam

3. Kezilahabi, E. (1979): *Gamba la Nyoka* Eastern African Publications

4. Mohamed, A.S. (1980): *Utengano*

5. Mohamed, M.S. (1978): *Nyota ya Rehema* OUP, Nairobi

6. Musokile, P.M. (198 ): *Thamani ya Ukubwa* DUP, Dar es Salaam

7. Mwana Charo, K. (1976): *Umelogwa au Umetumwa:* East African Literature Bureau, Nairobi

8. Mwaware, D.M. (1980): *Maputo* Longman Tanzania Ltd., Dar es Salaam

9. Robert, S. (1951): *Kusadikika* Thomas Nelson and Sons Ltd., London